# MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MJINI GEITA

# UTEKELEZAJI WA MIRADI MBALIMBALI YA MAENDELEO KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MITANO 2015 – 2020

**KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MITANO MAMLAKA IMEFANIKIWA KATIKA MAMBO YA YAFUTAYO;**

## 1. HALI YA UPATIKANAJI WA MAJI KATIKA MJI WA GEITA

Hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa wakazi wa Geita imeimarika kutoka **asilimia 3.1 mwaka 2015** mpaka **asilimia 65 Mwaka 2020** ya wakazi wote wa Mji wa Geita. Idadi ya wakazi wanaonufaika na huduma ya maji ni **158,291.**

Upande wa mtandao wa Mabomba Mamlaka imefanikiwa kuongeza utanuzi wa mtandao wa mabomba kutoka **kilometa 16.8 mwaka 2015 kilometa 270.226** mwaka 2020.

## 2. HALI YA HUDUMA YA MAJITAKA KATIKA MJI WA GEITA

Mamlaka imekamilisha ujenzi wa mtambo wa kisasa wa kutibu majitaka eneo la Usindakwe tofauti na awali ambapo majitaka hayo yalikuwa yakimwagwa kiholera katika maeneo yasiyo rasmi hivyo kuhatarisha uchafuzi wa mazingira.

## 3. MABORESHO YA UTOAJI WA HUDUMA

Mamlaka imefanikiwa kuratibu shughuli za utoaji huduma kwa kutumia mifumo ya kieletroniki kama vile kukokota maduhuri kwa kutumia mifumo, kutuma bili kwa kutumia meseji, kuanzisha dawati la huduma kwa wateja na simu ya bure ya wateja. Uanzishwaji huu wa mifumo hii imeimarisha mfumo wa mawasiliano baina ya Mamlaka na wateja.

## 4. **UTEKELEZAJI WA MIRADI MBALIMBALI YA MAENDELEO**

Katika kipindi cha miaka mitano 2015 -2020 Mamlaka imefanikiwa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo yenye thamani ya Tshs. **10,519,858,124.00** kama ilivyoainishwa katika jedwali Na. 1;

**Jedwali Na. 1. Idadi ya Watu Wanaopata huduma ya Maji**

| Mwaka | Idadi ya Watu | Mahitaji ya Maji (Mita za ujazo kwa siku) | Wakazi wanaopata Maji | % |
|---|---|---|---|---|
| 2015/2016 | 213,039 | 13,713 | 28,760 | 13.5 |
| 2016/2017 | 220,282 | 14,179 | 44,596 | 20.2 |
| 2017/2018 | 227,772 | 14,661 | 75,975 | 33.4 |
| 2018/2019 | 235,516 | 15,160 | 134,329 | 55 |
| 2019/2020 | 243,524 | 15,675 | 158,291 | 65 |

**Jedwali Na. 2: MIRADI YA MENDELEO ILIYOTEKELEZWA KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MITANO (2015 – 2020)**

| Na | Mradi | Muda wa Utekelezaji Mradi | Idadi ya Wanufaika | Gharama ya Mradi(TZS) | Fedha zilizotumika (TZS) | Mafanikio |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mradi wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira wa Ziwa Victoria MWAUWASA/LVWATSAN/EAC/W/2014/004 | Mei,2015 – Machi, 2019 | **135,000** | **6,664,871,353.00** | **6,169,281,398.00** | • Mradi huu umeongeza mtandao wa maji kwa **kilometa 54**,<br>• Uzalishaji wa maji kupitia visima virefu ongezeko la **lita 1,685,000** kwa siku.<br>• Ongezeko hili limepunguza mgawo maji kwa maeneo ya Kagera,Mkoani |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2 | | | | | | ,Ihayabuyaga na baadhi ya maeneo ya njia kuu iendayo Mwanza.<br>• Aidha mradi huu umewezesha ujenzi wa matenki ya kuhifadhia maji yenye **ujazo wa lita 815,000**.<br>• Mradi huu pia umetekeleza ujenzi wa miundombinu ya kisasa ya kutibu majitaka wastani wa **lita 500,000** kwa siku na Dampo la kisasa la kuchakata takangumu. Utekelezaji wa mradi huu umekamilika na unatumika. |
| 2 | Upanuzi wa mtandao wa usambazaji maji kwa Mji wa Geita | Agosti,2017-Machi,2018 | **20,000** | **296,225,904.00** | **288,593,178.1** | • Kazi imekamilika na mtandao wa maji umeanza kutumika.<br>• Mtandao huo wa maji umesaidia kufikisha |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | (GEUWASA/02/2016-17/HQ/W/01) | | | | | huduma ya maji kwa wakazi Zaidi ya 20,000. Mradi huu umeongeza mtandao wa maji kwa **kilometa 63.888** na kuwezesha wakazi wengi kuvuta maji kwa gharama nafuu. |
| 3 | Mradi wa maji Geita " Limited Distribution Network | Novemba,2014 – Mei, 2016 | 44,596 | **1,865,419,211.00** | **1,865,419,211.00** | • Mradi huu umeongeza uzalishaji wa maji wa mita za ujazo 3,500 – 4,200 kwa siku.<br>• Aidha umeongeza mtandao wa maji kilometa 41.3 |
| 4 | Mradi wa Ununuzi wa mabomba na Viungio (GEUWASA/02/2016-17/HQ/G/02) | Mei,2017– Novemba, 2017 | **20,000** | **855,714,111.00** | **855,714,111.00** | Ununuzi wa mabomba na viungio vyake umekamilika hivyo umewezesha zoezi la usambazaji wa maji **km 63.888** na maunganisho ya **wateja wapya 2,000.** |
| 5 | Mradi wa Ununuzi wa dira za maji | Mei,2017– Oktoba, 2017 | **20,000** | **136,968,020.00** | **136,968,020.00** | Uletaji wa dira za maji umekamilika hivyo umewezesha zoezi la |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | (GEUWASA/02/2016-17/HQ/G/01) | | | | | maunganisho ya wateja wapya 2,000. |
| 6 | Maunganisho ya maji kwa wateja wapya elfu mbili (GEUWASA/02/2016-17/HQ/W/02) | Desemba, 2017 – Machi,2019 | **20,000** | **127,086,000.00** | **114,377,453.09** | Mradi huu umefanikisha ongezeko la **wateja wapya 2,000**. |
| 7 | Ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mamlaka (GEUWASA/OB/W/2016-17/01) | June,2017 – Machi,2019 | **Wafanyakazi** | **396,103,529.25** | **377,067,351.01** | Ujenzi wa jengo umekamilika kwa asilimia **100** na jengo limeanza linatumika.<br>Kukamilika kwa jengo kumeimarisha motisha ya kufanya kazi hivyo kuongeza ufanisi katika utoaji huduma. |
| 8 | Mradi wa uletaji wa mabomba na Viungio (GEUWASA/AE/2018-19/G/01) | Tarehe ya kuanza 07/08/2019 – Tarehe ya Kukamilika 05/11/2019 Muda umeongezwa mpaka tarehe 15/12/2019 | **5,000** | **680,692,676.40** | **680,692,676.40** | • Ulazaji wa Mabomba umekamilika na baadhi ya wakazi wa maeneo yaliyopitiwa na mtandao wameshaanza kupata huduma ya maji. |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | • Kupitia mradi huu mtandao wa mabomba umeongezeka kwa **kilometa 30,** hivyo hali ya upatikanaji maji kwa wakazi wa mji wa Geita imeongezeka kutoka asilimia 55 mpaka asilimia 65. |
| 9 | Mradi wa Uboreshaji wa huduma ya maji Kasamwa | Tarehe ya Kuanza 5/4/2020<br>Tarehe ya Kumaliza 30/06/2020 | **5,000** | | | • Mamlaka imefanikiwa kukarabati visima viwili vya maji<br>• Mamlaka imefanikiwa kukarabati tenki la kuhifadhia maji lenye ujazo wa lita 60,000<br>• Mamlaka imefanikiwa kujenga vituo 5 vya kuchotea maji.<br>• Kwa sasa zoezi la utanuzi wa mtandao km 1.6 linaendelea sambamba na kuongeza vituo vipya 5. |

## 5. UTEKELEZAJI WA MRADI MKUBWA WA MAJI KUTOKA ZIWA VIKTORIA

Katika kipindi cha miaka mitano, Mamlaka imefanikiwa kuwepo katika miji 29 iliyopata kibali cha kutekeleza mradi mkubwa wa maji kupitia ufadhili wa masharti nafuu kutoka serikali ya India.

Mamlaka kwa kushirikiana na Kampuni ya WAPCOS imefanikiwa kukamilisha usanifu wa mradi .

Mradi huu kwa sasa upo katika hatua za mwisho za kumpata Mkandarasi wa ujenzi.

Naomba kuwasilisha.

Eng. Isaac Mgeni

**KNY:MKURUGENZI MTENDAJI**